



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

*Unapojibu tafadhali taja*

Kumb Na. HWB/C.40/34/169

Tarehe: 28 Disemba, 2021

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa kujaza nafasi za kazi katika kada ifuatayo;

### 1.0 MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA NAFASI MOJA (1)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa ya Kidato cha Nne au cha Sita na awe na Shahada ya Utawala au Sheria katika mojawapo ya fani za Utawala wa Umma au Sheria.
- Awe na uzoefu usiopungua miaka kumi (10) katika masuala ya Utawala na Sheria.

*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P. 59, BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.  
Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamoyode.go.tz](http://www.bagamoyode.go.tz)

## MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.
- (ii) Kuendesha vikao vyote vya Bodi ya Ajira kwa kufuata Kanuni, Sheria na Taratibu zilizopo.
- (iii) Kufungua vikao vya Bodi ya Ajira pamoja na Kufunga.

## MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe mwenyeji na mkazi wa Bagamoyo na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo.
2. Mwombaji awe na umri uliozidi miaka **60** na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V).
4. Maombi ya ambatishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (Kidato cha IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. Testimonial "provisional results" "statement of results" hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (FORM FOUR AND FORM SIX RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU

---

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P. 59, BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.

Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamoyode.go.tz](http://www.bagamoyode.go.tz)

na NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.

7. Waombaji waliostaafishwa kwa manufaa ya Umma katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba.
8. Hakutakuwa na mshahara kwa mwezi, Mwenyekiti wa Bodi atalipwa posho ya kikao kwa kila kikao kitakapofanyika.
9. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
10. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **20 Januari, 2022 saa 9:30 Alasiri.**
11. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta au kupitia Masjala ya Mkurugenzi kwa anwani ifuatayo: -

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo,  
S.L.P 59,

**BAGAMOYO-PWANI.**

Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz).



Shauri Selenda

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**BAGAMOYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
BAGAMOYO**

Tangazo hili linapatikana katika mbao za matangazo ofisi zetu za kata na tovuti: [www.bagamoyode.go.tz](http://www.bagamoyode.go.tz)